**HALMASHAURI YA WILAYA YA MAFIA**
**SHULE YA SEKONDARI KIRONGWE**

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI KIRONGWE,
S.L.P 70,
MAFIA.
Barua pepe.kirongwesekondaris1778@gmail.com.

Mobile na: **+255 787232317**
**+255 652730370**
**+255 787851747**
**+255 688594612**

---

**Kumb.Na. KRSS/UC.FV/VOL.03/……..**
MZAZI/MLEZI WA . ……………..……………………………………..

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA …………..**

Kwa niaba ya Bodi ya shule, watumishi na wanafunzi wote wa shule ya Sekondari Kirongwe, ninayo furaha kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha **TANO** katika shule ya sekondari **KIRONGWE**

**MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya Sekondari Kirongwe ipo wilayani Mafia katika mkoa wa Pwani. Usafiri wa kufika kisiwa cha Mafia unapatikana katika kituo cha mabasi cha MWANDEGE-Mkuranga barabara kuu kuelekea mkoa wa Lindi. Basi litakufikisha Nyamisati wilaya ya kibiti kwa gharama ya **Tshs.9,000/=** . Kisha Kutoka hapo utapanda Meli hadi Kilindoni-Mafia kwa gharama ya **Tshs. 16,000/=** Ambapo kuna usafiri wa gari 4000/=, pikipiki 10,000/= au bajaji 15,000/= umbali wa kilometa 24 hadi shuleni.

Kwa usafiri wa ndege kwenda Mafia, tunatumia kiwanja cha ndege cha JK-Nyerere terminal 1, Kwa nauli ya **Tshs. 160,000/=** kutoka Dar es salaam hadi Mafia, usafiri upo kila siku.

**Muda wa kuripoti ni kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni siku za jumatatu hadi jumapili katika ofisi ya malezi kwa maelekezo zaidi.**

**Muhula wa masomo unaanza tarehe ………… Hivyo, mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe …………… Mwisho wa kuripoti ni tarehe ………………………**

MAHITAJI YA LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI

Ni vyema mahitaji haya yatimizwe kabla ya kuanza safari ya kuja shuleni

A: Michango mbalimbali

| SN | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5000/= |
| 3 | Nembo | 5000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5000/= |
| | Jumla kuu kwa mwaka | 80,000/= |

Malipo yote yafanyike kupitia akaunti ifuatayo

Jina la akaunti: KIRONGWE SECONDARY RECURRENT ACCOUNT

A/C NO. 21501200195 NMB

HAKIKISHA UNAKUJA NA RISITI ZA MALIPO (PAY INSLIPS) INAYOONYESHA JINA LA MWANAFUNZI ALIYELIPIWA

- Mwanafunzi afike na godoro la futi 3x 6

NB: Mzazi hakikisha unamkatia mwanao bima ya afya

B. SARE ZA SHULE.

- WASICHANA.

i. Sketi mbili (2) za rangi ya **Dark blue** hakikisha inakuwa ndefu ya kugusa vifundo vya miguu (mshono wa rinda box)

ii. Sketi mbili za rangi ya **dark green** kwa ajili ya kushindia (SHAMBA DRESS)

iii. Hijabu (Juba) la rangi ya light bluu (bluu bahari) kwa wanafunzi wa kiislamu liwe ndefu inayofunika kifua kwa ajili ya kushindia (shamba dress)

iv. Mashati mawili (2) meupe ya mikono mirefu au brauzi yenye mikono mirefu (Nusu kanzu ndefu inayofunika makalio na isiyobana) kitambaa cha tetroni na kitambaa cha kichwani(hijabu) ndefu inayofunika kifua jozi mbili (2) kwa wanafunzi wa kiislamu

v. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika miguu jozi mbili(2) vya kamba na vinavyopigwa kiwi **sio vya plastic (Bajaj)
vi. Soksi nyeupe jozi mbili(2)
vii. Aje na T-Shirt mbili za kijivu panya zenye kola ( maarufu form six) za kushindia (shamba dress)
viii. Aje na sweta la rangi ya light bluu
ix. T-shirt ambayo ni sare ya shule (inapatikana shuleni). Mzazi atamnunulia mwanafunzi.
x. Aje na Tai ya rangi ya **dark blue**

- **WAVULANA.**

i. Suruali mbili (2) za rangi ya **dark blue** zenye mshono wa heshima wa Tanzania (zenye marinda mawili mbele, ndefu zinazofunika vifundo vya miguu, upana wa chini 14cm). Zingatia mshono hatapokelewa mwanafunzi kama atashona nje ya maelekezo.
ii. Suruali mbili za rangi ya **dark-green** kwa ajili ya kushindia zenye marinda mawili mbele (SHAMBA DRESS)
iii. Mashati mawili (2) meupe ya mikono mirefu
iv. Soksi nyeusi jozi mbili(2)
v. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika miguu jozi mbili(2) vya kamba na vinavyopigwa kiwi na visiwe na visigino virefu
vi. Mkanda mweusi usio na nembo za kihuni wala bakoli nene
vii. Aje na T-Shirt mbili za kijivu panya zenye kola (maarufu form six) za kushindia (shamba dress)
viii. Aje na sweta la rangi ya light bluu (**BLUU BAHARI**)
ix. T-shirt ambayo ni sare ya shule (inapatikana shuleni). Mzazi atamnunulia mwanafunzi.
x. Aje na Tai ya rangi ya dark blue

**C. SARE ZA MICHEZO**

**WAVULANA**

i. Aje na T-Shirt ya jezi ya Tanzania rangi ya blue na bukta yake
ii. Aje na tracksuit ndefu ya rangi ya light – blue **(BLUU BAHARI)**
iii. Aje na raba za michezo na vifaa vingine vya michezo

**WASICHANA**

i. Aje na T-Shirt ya jezi ya Tanzania rangi nyeupe
ii. Aje na tracksuit ndefu na isiyobana ya rangi ya light – bluu **(BLUU BAHARI)**
iii. **Sketi ya michezo nyeusi mzazi amshonee mtoto wake**
iv. Aje na raba za michezo na vifaa vingine vya michezo

**D: MAAGIZO MENGINE YA SHULE**

i. Cheti cha daktari (medical certificate) cha kuthibitisha afya ya mwanafunzi ambayo itajazwa na hospitali ya serikali

ii. Sanduku imara la kuhifadhia vifaa vyake

iii. Vyombo vya chakula (sahani,kijiko na kikombe)

iv. Ndoo za plastiki 2 za lita 10 kwa matumizi yake binafsi

v. Aje na chanzo cha mwanga kwa ajili ya tahadhari ya wakati wa usiku iwapo umeme utakosekana(**TOCHI**)

vi. Ream ( A4) mbili (2) kwa mwaka

vii. Vitabu vya masomo ya taasusi (combination) husika

viii. Shuka mbili za rangi moja (bluu bahari) na Mto wa kulalia

ix. Vifaa vya darasani kulingana na taasusi husika

x. Aje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya kazi za usafi

  a. **Jembe na kwanja kwa wavulana wote**

  b. **Panga na soft bloom (fagio laini) kwa wasichana wote**

xiv. Chandarua kimoja cha rangi ya blue

**E: MUHIMU:**

i. Mzazi/ Mlezi unashauriwa kumtimizia mwanao maagizo yote yanayohitajika na hakikisha kuwa **MWANAO ANAFIKA SHULENI KULINGANA NA TAREHE ILIYOPANGWA**

ii. Mzazi /Mlezi ahakikishe anaandika anuani ambayo itamuwezesha kupokea taarifa za maendeleo ya mwanae. Iwapo kutakuwa na mabadaliko yoyote ya anuani ni muhimu kutujulisha

Mwanao anatakiwa kutambua kuwa nafasi aliyoipata ni nyeti na adhimu hivyo anapaswa kuitumia nafasi hiyo kwa umakini wa hali ya juu ili baadae aweze kuwa na manufaa kwa familia, Jamii na taifa kwa ujumla.

ORODHA YA VITABU VYA MASOMO (Mzazi amnunulie mwanawe)

**HISTORY (Viwe vya mtaala mpya)**

1. History for Advanced secondary school students book Form five and six (TIE)

**GEOGRAPHY (Viwe vya mtaala mpya)**

1. Geography for Advanced secondary school students book Form five and six (TIE)

**KISWAHILI (Viwe vya mtaala mpya)**

1. Kiswahili shule za sekondari kitabu cha mwanafunzi kidato cha Tano na Sita (TIE)

**ENGLISH LANGUAGE (Viwe vya mtaala mpya)**

1. English language for Advanced secondary school students book Form five and six (TIE)

**HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI (Viwe vya mtaala mpya)**

1. Historia ya Tanzania na Maadili shule za sekondari kitabu cha mwanafunzi kidato cha Tano na sita (TIE)

**ACADEMIC COMMUNICATION SKILLS (Viwe vya mtaala mpya)**

1. Academic communication for Advanced secondary school students book Form five and six (TIE)

**MOTTO WA SHULE YETU NI "FUTURE IS OUR FOCUS"**

**KARIBU SANA KIRONGWE SEKONDARI.**

MOHAMED M. MSOSSOW

MKUU WA SHULE

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## PART A: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To: The Medical Officer (*Government Hospital)* **From: Kirongwe Secondary School,**

**………………………………………..** **P.O. Box 70,**

**………………………………………..** **Mafia.**

**………………………………………..** **Date……………………**

Mr/Mrs/Miss……………………………………………………… (Name in Full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full-time Secondary Education. The examination should include the following ineligible in case of a defect. Pregnancy (Category IV) will also render a girl candidate ineligible for a Secondary Education.

1. (a) Eye sight (b) Speech (c) Hearing (d) Limbs (e) Venereal Diseases (f) Leprosy (g) Epilepsy.
2. Neuroses 3. Other Serious diseases.

## Part B: MEDICAL CERTIFICATE:

1. (a) Eye sight:……………………………………………………………………………..
(b)Hearing:……………………………………………………………………………………
(c) Speech: ………. ……………………………………………………………………………..
(d) Limbs: ……… ……………………………………………………………………………..
(e) Venereal Diseases: ……………………………………………………………………..
(f) Leprosy: ……...………………………………………………………………………………
(g) Epilepsy: ……..……………………………………………………………………………..
(h) TB: ………. ………………………………………………………………………………...
2. Neuroses: ……..…………………………………………………………………………..
3. Pregnancy:…..……………………………………………………………………………..
4. Allergy ……………………………………………………………………………………………….
4. Other serious diseases:

..........................................................................................................................................

…………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

I have examined the above named, and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for full-time Secondary Education.

Designation: ………………………………………………………………. Date: ………………..

Signature & official Stamp:

*(To be completed by a Government Officer)*

***N.B: In case of any serious health problem (s), the records from the Government Hospital MUST be submitted to School when reporting.***

**F: SHERIA NA KANUNI ZA SHULE .**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha , inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais- TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu. Unazingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maadishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Mwanafunzi atasimama anapomsalimia mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri
2. Ni marufuku kwa mwanafunzi
    a. Kutumia lugha chafu au ya kihuni popote na wakati wowote
    b. Kupeleka au kulia chakula bwenini
    c. Kufuga kucha, ndevu na nywele
    d. Kunyoa kipara
    e. Kutia dawa nywele (curl) au kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa
    f. Kuvaa kofia shuleni au mapambo/urembo kama hereni, n.k. akiwa shuleni.
    g. Kuvaa viatu vya soli nene (ghorofa)
    h. Kuvaa kaptula, kandambili na fulana ya kukata mikono kwenye bwalo la chakula.
    i. Hairuhusiwi mwanafunzi kuja na nguo ambazo hazijaruhusiwa
    j. Kuja na silaha yoyote shuleni
    k. Pia haruhusiwi kutumia "chombo chochote cha umeme.
3. Atasimama kwenye mstari wakati wa kupata huduma.
4. LAZIMA mwanafunzi AWAHI NA AHUDHURIE mahali anapotakiwa katika shughuli za shule.
5. NI LAZIMA Mwanafunzi awe katika sare ya shule kwa nyakati zifiutazo:-
    a. Anapohudhuria masomo darasani.
    b. Anapotoka nje ya shule kwa ruhusa maalumu kwa shughuli yoyote itakayomlazimu kwenda nje ya shule.
6. NI LAZIMA mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya shule kwa ruhusa maalumu, na atapaswa kuwa na kibali (Pasi) cha maandishi.
7. Mwanafunzi lazima awe kitandani kwake wakati wa kuzima taa/kulala (lights out) saa 5.30 usiku.
8. Mwanafunzi haruhusiwi:-
    i. Kwenda kwenye nyumba za watumishi wa shule bila kibali maalum.
    ii. Kuingia kwenye Ofisi za Shule – Ofisi za walimu, jikoni, na maabara bila ruhusa.
9. USAFI: Mwanafunzi anawajibika kuwa msafi na kushiriki kuyaweka mazingira ya shule katika hali ya usafi

**MUHIMU:**

***Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile,na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.***

***Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa shule.(Msiba au Ugonjwa)***

**G: MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE:**

a) Wizi wa aina yoyote ile ilimradi ushahidi upo

b) Uasherati na Ushoga.

c) Ubakaji.

d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji sigara na bangi, cocaine, mirungi, kubeli, na kadhalika

e) Kupigana au kupiga.

f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

g) Kudharau bendera ya Taifa, wimbo wa taifa

h) Kuwa mjamzito/ Kupata mimba/ kusababisha mimba

i) Kutoa mimba

j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

k) Kukataa adhabu kwa makusudi.

l) kumiliki au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

m) kuwa na mahusiano ya kimapenzi

n) Kukutwa nje ya eneo la shule bila kibali

## TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. i) Jina kamili la mwanafunzi……………………………………………………………………………………Me/Ke

ii) Tarehe ya kuzaliwa……….. mwezi………..mwaka……………..………………...

iii) Shule uliyotoka kidato cha Nne;……………………………………………………

Anwani………………………………………………..…….………………….

2. Je wazazi wote ni hai? Ndiyo / hapana………………….…….……………………..

a) Na kama hapana nani yuko hai …………………………………………………

Jina la mzazi (wazazi)……………………………..……………………..

Kazi yake: ………………………………………………………………..

Anuani yake: ……………………………………………..……………..

Makazi yake : ………………………Simu:………………………………

b) Kama unalelewa na mlezi asiye mzazi wako;

Jina la mlezi wako (majina matatu)…………………………………………

Uhusiano na mlezi wako (kaka,dada,n.k)…………………………..…………

Kazi yake………………………………………………………………..

Anwani yake……………………………………………...……………..

Makazi yake: …………………………..Simu……………………………..

3. Afya.

a) Je una ulemavu wa viungo? Ndiyo /hapana……………..…………………..

b) Kama ndiyo taja aina ya ulemavu………………………………..……….

5. Uthibitisho wa taarifa iliyotolewa;

Mimi (jina la mwanafunzi) ………………………………………………..nathibitisha kwamba maelezo niliyotoa ni ya KWELI na endapo itathibitika kuwa nimedanganya hatua stahiki za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.

Tarehe………..…………….. Sahihi…………..……………….………………..

6 Jina na sahihi ya mzazi/mlezi

Jina…………….……………………… Sahihi……………..………………